zebra

Child Protection Centre

# Kituo cha Zebra:

Mwongozo wa hatua kwa hatua

# YALIYOMO

Kituo cha Zebra cha ulinzi wa watoto (The Zebra Child Protection Centre) kilikuwa ndicho kituo cha kipekee na cha kwanza cha kutetea haki za watoto na vijana ambao wamepitia dhulma. Timu yetu ya kimataifa iliyo na wafanyikazi wa Kituo cha Zebra na wanaojitolea, Huduma ya Polisi ya Edmonton, RCMP, Huduma za watoto, na Huduma za Afya za Alberta, inafanya kazi
kusaidia watoto wakati wote wa utunzaji - pamoja na kufichua yote, uchunguzi, mwendo wa mahakama na uponyaji.

Mwongozo huu utakupa mwelekezo kufika Kituo cha Zebra, kipi cha kutarajia unapofika, mwendo wa mahojiano ulivyo, habari muhimu kwa jukumu lako kama mlezi na habari ya mawasiliano ili utufikie iwapo una maswali au hoja.
Utaweza pia kupokea habari na rasilimali unapofika katika kituo.


Tahadhari ya COVID-19 **3**

Jinsi ya kufika katika kituo **4**

Kufika kwenye Kituo **5**

Utaratibu wa mahojiano **6**

Habari muhimu **7**




**Kituo cha Zebra kinachukulia tahadhari kusaidia kupunguza kuenea kwa janga ya COVID-19. Kwa hivyo,tumetekeleza,tahadhari zifuatazo:**

- Wageni wote wanahitajika kuvaa barakoa wakiwa kwenye kituo cha Zebra. Iwapo hawana barakoa,watapewa moja watakapo fika.
- Tafadhali fika dakika kumi kabla ya miadi yako. Utakapofika mapema zaidi ya dakika kumi,tafadhali ngoja uwanjani katika sakafu kuu hadi wakati wa miadi yako.
- Tafadhali tusaidie kupunguza idadi ya watu katika kituo kwa kuja tuu na wale ambao ni muhimu kwenye miadi yako.
- Tafadhali ambatana na umbali wa mwili na ufuate alama za mwelekeo.
- Iwapo unajihisi mgonjwa ,tafadhali usije kwa miadi yako,fuata mapendekezo ya Huduma za Afya za Alberta(AHS).
- Wafanyi kazi wote watavaa barakoa katika nafasi zote za umma na kote katika kituo.
- Tunanyunyizia dawa na kusafisha eneo la mahojiano na vyumba vyenye urafiki wa watoto na nafasi za kawaida baada ya kila familia.
- Mara kwa mara tuna nyunyizia na kusafisha nafasi na sehemu zinazo guswa sana kote katika kituo.

**Utaulizwa maswali yafuatayo kuhusiana na COVID –19.**

1. Je, unaonyesha dalili zozote za ugonjwa?(joto jingi mwilini,kukohoa, upungufu wa pumzi na kulemewa na kupumua )
2. Je, umepimwa,unangoja matokeo yako au umepanga kupimwa ugonjwa wa COVID-19?
3. Je, umesafiri nje ya taifa la Canada kwa muda wa siku kumi na nne zilizopita?
4. Je, umemkaribia mtu yeyote aliyepimwa na ugonjwa au dalili zozote za COVID – 19?
5. Je, umemkaribia mtu yeyote aliye na ugonjwa wa kupumua ambaye amesafiri popote nje ya Canada kwa muda wa siku kumi na nne kabla ya ugonjwa wake?
6. Je, umehusika na maabara yenye nyenzo za kibaolojia(kwa mfano. viashiria vya kliniki vya msingi,viungi vya virusi)zinazojulikana kuwa na virusi vya COVID-2019
7. Je, kuna yeyote nyumbani kwako aliye na joto jingi au anyekohoa au aliye na umpungufu wapumzi aliye kuwa amesafiri popote nje ya Canada kwa muda wa siku kumi na nne kabla ya kuugua?
8. Je, unangoja matokeo yako baada ya kupimwa ugonjwa wa COVID-19?



# MAEGESHO YA KITUO CHA ZEBRA




Maegesho katika Kituo cha Zebra yanapatikana **mwisho wa kusini** wa uwanja (WSP Place 10909 Jaspe Avenue). unaweza kupata maegesho kwa kuenda kusini kwenye **109 Street Nw** kulekea **100Ave Nw**.Pinduka **kulia** baada ya bodi ya elektroniki jinsi inavyo onyeshwa kwenye picha iliyo kushoto.

Tunazo nafasi sita **(nafasi #17 hadi #22)** zilizo na number zinazoonyesha kwenye sanduku nyeupe.Tafuta alama zilizo kwenye vizuizi vya simiti vinavyo kaa hivi:




Andikisha namba ya nafasi ulioweka gari lako na namba ya usajili ya gari lako katika mapokezi.Gari ambazo hazijaegeshwa katika nafasi hizi ziko kwenye hatari ya kuvutwa kwa gharama ya mwenye gari.

# JINSI YA KUTUPATA




1



2





3

Kuingia kwa kituo cha WSP ni upande wa kushoto wa Jumba Kuu la Jamii (picha 1).

Tupo katika ghorofa ya saba ya jumba hili.Utakapo fika,pinduka kushoto na utauona mlango ulio na mchoro wa pundamilia nyuma yake.(picha 2)

Mara tu ukifika ndani,nenda kwenya mlango ulioko kushoto na upige kengele ilio kwenye duara la kijani ili uweze kuingia kwenye mapokezi.(picha 3).







## MAPOKEZI

Mara tu ukifika mapokezi, mshiriki wa timu ya Kituo cha Zebra atakuwa huko kukusalimu.

.

Maelezo yako ya maegesho ya gari lako yatakusanywa kwa wakati huu.

## VYUMBA VYENYE URAFIKI WA WATOTO

Hapa mtoto wako anaweza kucheza,kupaka rangi an apumzike kabala ya mahojiano.

Mmoja wa watetezi wetu wa watoto atafuatana na wewe na mtoto wako kwenye moja ya vyumba vyenye urafiki wa watoto.

Mtetezi atakuwa hapo ili aweza kukupa msaada na kujibu maswali.

## MBWA WA OFISI

Katika kituo cha Zebra kunae FLETCHER ambaye ni mbwa anaeitwayupo hapa ili awape msaada wa kihemko watoto katika kituo na pia kortini.

Fletcher anaweza kupatikana kituoni, kukutana na kusakimiana na mwanao. Iwapo wewe ama mwanao hamtaki Mbwa awepo,unaweza kuchagua na kuamua hivyo

.

** Tafadhali zingatia kuwa Kwa wakati huu Fletcher hapatikani kuwasalimu na kukutana katika kituo kwa sababu ya COVID-19.**



## MAHOJIANO

Mpelelezi au mhojiwa wa uchunguzi atampeleka mtoto wako kwenye chumba cha mahojiano, ambacho kina vifaa vya kamera na maikrofoni. Huko, watafanya mahojiano ya kizazi na mtoto kuhusu tukio katika nafasi salama na starehe.



## BAADA YA MAHOJIANO

Afisa anayesimamia faili ya mtoto wako atajadili hatua zifuatazo za uchunguzi baada ya mahojiano (hatua hizi zitatofautiana kulingana na matokeo ya mahojiano).

Mawakili wa watoto watakupasha na habari inayofaa na marejeleo kupitia simu.

Zingatia mahitaji ya kihemko ya mtoto wako, lakini usifanye mazungumzo marefu na mtoto wako kuhusu uzoefu. Zingatia ufunuo wowote wa ziada.

# MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Ni bora **kutojadili mahojiano** kabla ya kuja kwenye Kituo kwani wachunguzi watataka **kujua kabisa** hadithi ya mtoto isiyo na **kuficha au kuchongwa** wakati wanahojiwa.

Kesi zingine zimepewa kipaumbele kwa kuzingatia usalama wa mtoto na familia, utunzaji wa ushahidi, na hatari inayosababishwa na mshukiwa kwa familia na umma kwa ujumla. Kama hivyo, kila kesi ni tofauti na itachukua muda tofauti kufungwa. Walezi wengi wanapaswa kujua kuwa inaweza kuchukua miezi kadhaa kabla ya uchunguzi kufungwa.

Mtoto wako anaweza kutoonyesha wakati wa mchakato wa mahojiano, na hiyo ni sawa. Muulize afisa anayesimamia kama au azungumze juu ya tukio hilo na mtoto wako. Watoto wengine wanaweza kuwa hawako tayari kufichua, na kwa kuwa hakuna kikomo cha wakati juu ya mashtaka ya makosa ya kijinsia, ni bora kwa mtoto kuchukua wakati wao kufichua.

# ANWANI ZA OFISI

Utaweza pata hapa chini habari muhimu ya mawasiliano yetu. Tafadhali uwe huru kutufikia sisi au afisa wa polisi aliyepewa kisa cha mtoto wako ikiwa una maswali au wasiwasi wowote wakati wowote.

**MAPOKEZI YA KITUO CHA ZEBRA**

780. 421. 2385

**BARUA PEPE**

info@zebracentre.ca

**TOVUTI**

zebracentre.ca

**NAMBARI YA MSAADA WA FAMILIA**

(Iwapo mapokezi hayapatikani)

780. 421. 2359